



Misitu ya Jamii Tanzania Uthibitishaji wa Pamoja

Meneja wa Umoja: +255 (0)23 201 3093 au tzfmc-group-manager@mpingoconservation.org

KANUNI KUU NA VIGezo VYA UTHIBITISHAJI MISITU

Ili msitu uweze kuthibitishwa kwamba unasimamiwa na kutunzwa kiendelevu, ni lazima kanuni zifuatazo zizingatiwe na kutimizwa. Kanuni hizi ni vigezo muhimu vilivyowekwa na taasisi ya uthibitishaji misitu itwayo **Forest Stewardship Council (FSC)**.

Kuna jumla ya kanuni kuu kumi, lakini kanuni na vigezo vinavyoendana na mazingira yetu ni tisa tu ambazo ni:-

Kanuni ya 1: Kutimiza Sheria na Matakwa ya FSC

- Usimamizi misitu lazima uheshimu na kuzingatia sheria zote za nchi zinazotumika pamoja na mikataba yeyote ya kimataifa ambayo nchi imesaini. *Kwa mfano sheria ya misitu ya mwaka 2002, Sera ya misitu ya mwaka 1998 na miongozo mbalimbali.*
- Usimamizi misitu lazima uheshimu sheria za kitaifa, sheria ndogo na mahitaji ya kiutawala. *Mfano sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982, sheria ndogo za vijiji na sheria ndogo za Halmashauri ya Wilaya.*
- Ushuru, kodi na malipo mengine yanayotambulika kisheria ni lazima yalipwe.
- Serikali za vijiji vitalipa kodi ya mapato na kodi ya ongezeko la thamani (VAT).
- Misitu ya jamii lazima ilindwe dhidi ya uvunaji haramu, makazi msituni na shughuli zozote zisizoruhisiwa.
- Usimamizi misitu ni lazima uonyeshe nia ya kufuata masharti ya FSC kwa kipindi kirefu.

Kanuni ya 2: Kumiliki Ardhi, Haki ya Matumizi na Majukumu

- Umiliki wa ardhi wa kudumu, haki ya kutumia ardhi na rasilimali za misitu ni lazima ibainishwe na kuonyeshwa kisheria. *Hii imebainishwa katika mpango wa usimamizi misitu.*
- Vielelezo vya kumiliki ardhi kwa muda mrefu ni sharti viwepo. *Kama vile cheti cha ardhi, hati ya kumiliki ardhi, umiliki wa kimila/jadi.*

Kanuni ya 3: Haki ya Wakazi

- Haki ya wanajamii kumiliki, kutumia na kusimamia ardhi na maliasili ni lazima zitambuliwe na kuheshimiwa. *(Zimebainishwa katika mpango wa usimamizi misitu.)*
- Usimamizi misitu usihatarishe umiliki wa ardhi ya wakazi kwa namna yeyote ile.
- Maeneo maalum ya jamii kwa ajili ya kijadi, kidini na mengineyo ni lazima yabainishwe kwa kuwashirikisha wahusika wa maeneo hayo na ni sharti yaheshimiwe. *(Kuna kipengele hiki mpango wa usimamizi misitu.)*

Kanuni ya 4: Mahusiano ya Kijamii

- Shughuli za usimamizi misitu ni lazima zizingatie masilahi ya muda mrefu ya kiuchumi na kijamii kwa wanajamii.
- Usimamizi misitu ni lazima uchukue taadhari dhidi ya kuleta madhara ya aina yeyote ile kwa wanajamii.
- Hatua muhimu ni lazima zichukuliwe ili kusuluhisha pale panapokuwa na migongano kuhusiana na usimamizi misitu.

Kanuni ya 5: Faida za Misitu

Shughuli za usimamizi misitu ni sharti zitilie mkazo matumizi bora ya rasilimali za misitu na huduma zinginezo zitokanazo na misitu ili kuwepo faida za kiuchumi, kimazingira na kijamii

Kanuni ya 6: Madhara ya Kimazingira

- Usimamizi misitu ni sharti uzingatie uhifadhi wa bioanuwai/viumbe vyote vilivyopo msituni, vyanzo vya maji, udongo na mazingira kwa ujumla.
- Iwapo kuna maeneo muhimu kwa viumbe kama vile mazalia ya ndege ni sharti yasiathiriwe na shughuli za usimamizi misitu.
- Takakata zote na mabaki mengine ni lazima yatupwe nje ya msitu. *Mfano karatasi, makopo ya rangi, mabaki mengine wakati wa kufanya kazi msituni.*
- Matumizi ya madawa ya kemikali hayaruhusiwi msituni. *Mfano mbolea za kukuzia.*
- Matumizi ya jamii za miti isiyo ya asili ni budi yakadhibitiwa.

Kanuni ya 7: Mpango wa Usimamizi

- Mpango wa Usimamizi misitu lazima uandaliwe, utekelezwe na urekebishwe ili uendane na wakati. Malengo ya muda mrefu ya mpango na jinsi ya kuyafikia malengo hayo ni lazima yabainishwe.
- Pamoja na vitu vingine ramani ya msitu na zinginezo muhimu lazima ziambatanishwe katika mpango.
- Mpango wa Usimamizi lazima urekebishwe mara kwa mara ili kujumuisha mabadiliko yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi, ushauri wa kitalaam na mabadiliko ya kimazingira, kijamii na kiuchumi. *(Imebainishwa kuwa mpango wa usimamizi unaweza kurekebishwa kila baada ya miaka mitano.)*

Kanuni ya 8: Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na tathmini ni lazima ufanyike ili kubaini hali ya msitu, mazao ya misitu, kazi za usimamizi na madhara ya kijamii na kimazingira. *MCP itafanya na wanajamii kwa ujumla watafanya tathmini mara kwa mara ili kubaini mabadiliko ya hali ya msitu; tathmini pia itafanywa na wathibitishaji kila mwaka.*

Kanuni ya 9: Uhifadhi wa Misitu Muhimu

Uhifadhi wa viumbe na mimea iliyohatarini kutoweka na isiyopatikana mahali pengine duniani lazima uzingatiwe. *Eneo lenye ukubwa wa 10% ya msitu kwa ajili ya uhifadhi tu na ambalo halitavunwa limetengwa.*